

**KUMB: PPR/19 - 10/1**

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA BIDHAHA ZA MAFUTA YA PETROLI  
KUANZIA JUMATANO, TAREHE 2 OKTOBA 2019**

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 2 Oktoba 2019**. Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchi nzima, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

- (a) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya **Dar es Salaam**, zimepungua ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 4 Septemba 2019. Kwa mwezi Oktoba 2019, bei za rejareja za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimepungua kwa Shilingi 142/lita (sawa na asilimia 6.34), Shilingi 59/lita (sawa na asilimia 2.72) na Shilingi 77/lita (sawa na asilimia 3.59), mtawalia. Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimepungua kwa Shilingi 141.34/lita (sawa na asilimia 6.69) na Shilingi 58.78/lita (sawa na asilimia 2.88) na Shilingi 76.29/lita (sawa na asilimia 3.80), mtawalia. Kupungua kwa bei za mafuta katika soko la ndani kwa mafuta yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Dar es Salaam kunatokana na kushuka kwa bei za mafuta katika soko dunia kama inavyoonekana katika **Jedwali C**.
- (b) Kwa mwezi Oktoba 2019, bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa kwa **Mikoa ya Kaskazini** (Tanga, Arusha, Kilimanjaro na Manyara) zitaendelea kuwa zile zilizotangazwa katika toleo lililopita la tarehe 4 Septemba 2019. Hii ni kutokana na kwamba, kwa mwezi Septemba 2019, hakuna shehena ya mafuta iliyopokelewa nchini kupitia bandari ya Tanga.
- (c) Vilevile, kwa mwezi Oktoba 2019, bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli na Dizeli kwa **Mikoa ya Kusini** (Lindi, Mtwara na Ruvuma) zitaendelea kuwa zile zilizotangazwa katika toleo lililopita la tarehe 4 Septemba 2019. Hii ni kutokana na kwamba, kwa mwezi Septemba 2019, hakuna shehena ya mafuta iliyopokelewa nchini kupitia bandari ya Mtwara. Aidha, kwa kuwa hakuna Mafuta ya Taa yaliyopokelewa katika bandari ya Mtwara, wamiliki wa vituo vya mafuta katika mikoa tajwa wanashauriwa kununua mafuta hayo kutoka Dar es Salaam na hivyo bei za rejareja za Mafuta ya Taa kwa mikoa hiyo zinatokana na gharama za mafuta hayo kutokea Dar es Salaam na kusafirishwa hadi mkoa husika.
- (d) EWURA inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za mafuta kwa eneo husika, zinapatikana pia kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba **\*152\*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.
- (e) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau

kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.

- (f) **Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hizo zisivuke bei kikomo (*price cap*) kama ilivyokokotolewa na kanuni (*formula*) iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapishwa katika **Gazeti la Serikali Na. 163 la mwezi Aprili 2018 na Gazeti la Serikali Na. 269 la mwezi Juni 2018.****
- (g) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**
- (h) Wauzaji wa mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa risiti za mauzo kutoka kwenye mashine za EFPP (*Electronic Fiscal Pump Printers*) na Wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo za malipo zitatumika kama kidhibiti kwa wanunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya aidha kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora kinachofaa, na pia, risiti hizo zitasaidia kurahisisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mauzo ya mafuta ya petroli.

#### JEDWALI A: BEI ZA REJAREJA

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta Ya Taa (Shs/Lita)
<b>Dar es Salaam</b>	<b>2,094</b>	<b>2,109</b>	<b>2,056</b>
<b>Arusha</b>	<b>2,356</b>	<b>2,259</b>	<b>2,123</b>
Arumeru (Usa River)	2,356	2,259	2,123
Karatu	2,375	2,278	2,141
Longido	2,367	2,270	2,134
Monduli	2,362	2,265	2,129
Monduli-Makuyuni	2,366	2,269	2,133
Ngorongoro (Loliondo)	2,441	2,344	2,208
<b>Pwani (Kibaha)</b>	<b>2,099</b>	<b>2,114</b>	<b>2,060</b>
Bagamoyo	2,105	2,120	2,067
Chalinze Junction	2,108	2,124	2,070
Chalinze (Msata)	2,113	2,128	2,074
Kibiti	2,115	2,130	2,076
Kisarawe	2,101	2,116	2,063
Mkuranga	2,104	2,119	2,066
Rufiji	2,122	2,137	2,083
<b>Dodoma</b>	<b>2,153</b>	<b>2,168</b>	<b>2,115</b>
Bahi	2,160	2,175	2,122
Chamwino	2,148	2,163	2,110

Chemba	2,179	2,195	2,141
Kondo	2,186	2,201	2,147
Kongwa	2,150	2,165	2,112
Mpwapwa	2,154	2,169	2,116
Mtera (Makatopora)	2,172	2,187	2,133
<b>Geita</b>	<b>2,260</b>	<b>2,275</b>	<b>2,221</b>
Bukombe	2,249	2,264	2,210
Chato	2,281	2,296	2,242
Mbogwe	2,298	2,313	2,259
Nyang'hwale	2,275	2,290	2,236
<b>Iringa</b>	<b>2,158</b>	<b>2,173</b>	<b>2,120</b>
Ismani	2,163	2,179	2,125
Kilolo	2,163	2,178	2,124
Mufindi (Mafinga)	2,168	2,184	2,130
<b>Kagera (Bukoba)</b>	<b>2,310</b>	<b>2,325</b>	<b>2,271</b>
Biharamulo	2,284	2,299	2,246
Karagwe (Kayanga)	2,326	2,341	2,288
Kyerwa (Ruberwa)	2,332	2,347	2,293
Muleba	2,310	2,325	2,271
Ngara	2,298	2,313	2,259
Misenyi	2,318	2,333	2,280
<b>Katavi (Mpanda)</b>	<b>2,302</b>	<b>2,317</b>	<b>2,264</b>
Mlele (Inyonga)	2,284	2,299	2,246
Mpimbwe (Majimoto)	2,295	2,310	2,257
Tanganyika (Ikola)	2,320	2,335	2,282
<b>Kigoma</b>	<b>2,326</b>	<b>2,341</b>	<b>2,287</b>
Uvinza (Lugufu)	2,338	2,353	2,299
Buhigwe	2,315	2,330	2,276
Kakonko	2,283	2,298	2,244
Kasulu	2,312	2,327	2,273
Kibondo	2,290	2,305	2,252
<b>Kilimanjaro (Moshi)</b>	<b>2,346</b>	<b>2,249</b>	<b>2,113</b>
Hai (Bomang'ombe)	2,349	2,252	2,116
Mwanga	2,339	2,242	2,106
Rombo (Mkuu)	2,363	2,266	2,129
Same	2,332	2,235	2,099
Siha (Sanya Juu)	2,352	2,255	2,119
<b>Lindi</b>	<b>2,331</b>	<b>2,236</b>	<b>2,115</b>
Lindi-Mtama	2,336	2,240	2,133
Kilwa Masoko	2,355	2,260	2,090
Liwale	2,367	2,271	2,136
Nachingwea	2,351	2,256	2,144
Ruangwa	2,357	2,262	2,146
<b>Manyara (Babati)</b>	<b>2,390</b>	<b>2,293</b>	<b>2,157</b>
Hanang (Katesh)	2,401	2,304	2,168
Kiteto (Kibaya)	2,406	2,309	2,172
Mbulu	2,403	2,306	2,170
Simanjiro (Orkasumet)	2,422	2,325	2,189

<b>Mara (Musoma)</b>	<b>2,273</b>	<b>2,288</b>	<b>2,234</b>
Musoma Vijijini (Busekela)	2,314	2,329	2,275
Rorya (Ingirijuu)	2,282	2,297	2,243
Rorya (Shirati)	2,316	2,332	2,278
Bunda	2,264	2,279	2,226
Bunda (Kisorya)	2,274	2,289	2,235
Butiama	2,270	2,285	2,231
Serengeti (Mugumu)	2,318	2,334	2,280
Tarime	2,284	2,299	2,245
Tarime (Kewanja/Nyamongo)	2,288	2,304	2,250
<b>Mbeya</b>	<b>2,201</b>	<b>2,216</b>	<b>2,163</b>
Chunya	2,211	2,226	2,172
Chunya (Makongolosi)	2,225	2,240	2,187
Kyela	2,217	2,232	2,179
Mbarali (Rujewa)	2,185	2,201	2,147
Rungwe (Tukuyu)	2,210	2,225	2,172
<b>Morogoro</b>	<b>2,119</b>	<b>2,134</b>	<b>2,081</b>
Mikumi	2,135	2,150	2,096
Kilombero (Ifakara)	2,157	2,172	2,119
Kilombero (Mlimba)	2,179	2,195	2,141
Kilombero (Mngeta)	2,169	2,184	2,130
Ulanga (Mahenge)	2,168	2,183	2,129
Malinyi	2,178	2,193	2,140
Kilosa	2,138	2,153	2,099
Gairo	2,138	2,153	2,099
Mvomero (Wami Sokoine)	2,130	2,145	2,091
Mvomero (Sanga Sanga)	2,119	2,134	2,081
Turiani	2,144	2,159	2,106
<b>Mtwara</b>	<b>2,317</b>	<b>2,222</b>	<b>2,128</b>
Nanyumbu (Mangaka)	2,354	2,258	2,177
Masasi	2,334	2,238	2,154
Newala	2,338	2,243	2,160
Tandahimba	2,331	2,236	2,153
Nanyamba	2,331	2,236	2,153
<b>Mwanza</b>	<b>2,244</b>	<b>2,259</b>	<b>2,206</b>
Kwimba	2,262	2,277	2,224
Magu	2,252	2,268	2,214
Misungwi	2,239	2,254	2,200
Sengerema	2,277	2,292	2,238
Ukerewe	2,304	2,319	2,265
<b>Njombe</b>	<b>2,187</b>	<b>2,202</b>	<b>2,148</b>
Njombe (Kidegembye)	2,207	2,222	2,169
Ludewa	2,225	2,240	2,186
Makambako	2,179	2,194	2,141
Makete	2,217	2,233	2,179
Wanging'ombe (Igwachanya)	2,184	2,200	2,146
<b>Rukwa (Sumbawanga)</b>	<b>2,267</b>	<b>2,282</b>	<b>2,229</b>
Sumbawanga Rural (Mtowisa)	2,267	2,282	2,229

Kalambo (Matai)	2,274	2,290	2,236
Nkasi (Namanye)	2,281	2,296	2,242
<b>Ruvuma (Songea)</b>	<b>2,403</b>	<b>2,308</b>	<b>2,179</b>
Mbinga	2,416	2,320	2,213
Namtumbo	2,394	2,299	2,209
Nyasa (Mbamba Bay)	2,441	2,346	2,223
Tunduru	2,368	2,273	2,238
<b>Shinyanga</b>	<b>2,223</b>	<b>2,238</b>	<b>2,185</b>
Kahama	2,237	2,252	2,198
Kishapu	2,252	2,267	2,213
Ushetu (Nyamilangano)	2,254	2,270	2,216
Simiyu (Bariadi)	2,265	2,280	2,226
Busega (Nyashimo)	2,258	2,273	2,219
Itilima (Lagangabilili)	2,268	2,283	2,229
Maswa	2,256	2,271	2,218
Meatu (Mwanhuzi)	2,263	2,278	2,225
<b>Singida</b>	<b>2,185</b>	<b>2,200</b>	<b>2,147</b>
Iramba	2,197	2,212	2,159
Manyoni	2,169	2,185	2,131
Ikungi	2,180	2,196	2,142
Mkalama (Nduguti)	2,209	2,225	2,171
<b>Songwe (Vwawa)</b>	<b>2,211</b>	<b>2,226</b>	<b>2,172</b>
Songwe (Mkwajuni)	2,217	2,233	2,179
Ileje	2,214	2,230	2,176
Momba (Chitete)	2,220	2,235	2,181
Tunduma	2,215	2,230	2,176
<b>Tabora</b>	<b>2,248</b>	<b>2,264</b>	<b>2,210</b>
Igunga	2,202	2,218	2,164
Kaliua	2,267	2,283	2,229
Ulyankulu	2,262	2,277	2,223
Nzega	2,213	2,228	2,175
Sikonge	2,260	2,275	2,222
Urambo	2,262	2,277	2,223
Uyui	2,249	2,265	2,211
<b>Tanga</b>	<b>2,300</b>	<b>2,203</b>	<b>2,066</b>
Handeni	2,320	2,223	2,087
Kilindi	2,335	2,238	2,102
Korogwe	2,312	2,215	2,079
Lushoto	2,321	2,224	2,088
Mkinga (Maramba)	2,307	2,210	2,073
Muheza	2,304	2,207	2,071
Pangani	2,306	2,209	2,073

**JEDWALI B: BEI KIKOMO KWA BEI ZA JUMLA**

	<b>Petroli (Shs/Lita)</b>	<b>Dizeli (Shs/Lita)</b>	<b>Mafuta ya Taa (Shs/Lita)</b>
<b>DAR ES SALAAM</b>	<b>1,970.55</b>	<b>1,985.30</b>	<b>1,932.57</b>
<b>TANGA</b>	<b>2,175.36</b>	<b>2,078.33</b>	<b>1,943.21</b>
<b>MTWARA</b>	<b>2,193.14</b>	<b>2,097.91</b>	<b>-----</b>

**JEDWALI C: SABABU ZA MABADILIKO YA BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA NDANI****BANDARI YA DAR ES SALAAM**

	<b>Petroli</b>	<b>Dizeli</b>	<b>Mafuta ya Taa</b>
<b>Mabadiliko ya Bei za mafuta katika soko la dunia</b>	Punguzo la Dola 62.534/Tani	Punguzo la Dola 23.557/Tani	Punguzo la Dola 17.665/Tani
<b>Mabadiliko ya gharama za usafirishaji (BPS premiums)</b>	Ongezeko la Dola 0.690/Tani	Punguzo la Dola 1.513/Tani	Punguzo la Dola 6.630/Tani

**JEDWALI D: BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA DUNIA ZILIZOTUMIKA KUKOKOTOA BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA NDANI**

	<b>Bandari</b>	<b>Petroli</b>	<b>Dizeli</b>	<b>Mafuta ya Taa</b>
<b>Mafuta yalipokelewa mwezi wa:</b>	<b>DSM</b>	Septemba 2019	Septemba 2019	Septemba 2019
	<b>Tanga</b>	Agosti 2019	Agosti 2019	Julai 2019
	<b>Mtwara</b>	Agosti 2019	Agosti 2019	n/a
<b>Wastani wa bei za mafuta katika soko la dunia kwa mwezi:</b>	<b>DSM</b>	Agosti 2019	Agosti 2019	Agosti 2019
	<b>Tanga</b>	Julai 2019	Julai 2019	Juni 2019
	<b>Mtwara</b>	Julai 2019	Julai 2019	----
<b>Wastani wa bei za mafuta katika soko la dunia kwa miezi inayoonekana hapo juu inalinganishwa na wastani wa bei za mwezi:</b>	<b>DSM</b>	Julai 2019	Julai 2019	Julai 2019
	<b>Tanga</b>	Julai 2019	Julai 2019	Juni 2019
	<b>Mtwara</b>	Julai 2019	Julai 2019	----

**Nzinyangwa E. Mchany**  
**KAIMU MKURUGENZI MKUU**  
**EWURA**